JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

**KATIKA KAMATI YA MAUDHUI YA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA, DAR ES SALAAM**

**MASHTAKA YA UKIUKAJI WA KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA (MAUDHUI YA MITANDAONI), 2018**

**SHAURI NA. 10 - 2018/2019**

# GILLY BONNY ONLINE TV

# UAMUZI

**UAMUZI WA KAMATI YA MAUDHUI KUHUSU TUHUMA YA UKIUKAJI WA KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA (MAUDHUI YA MITANDAONI), 2018.**

## 1.0 Utangulizi

**1.1** Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilitoa leseni ya kutoa maudhui mtandaoni kwa **GILLY BONNY ONLINE TV**, kwa ajili ya kuchapisha na kutangaza habari mbali mbali mitandaoni.

**1.2** Kwa mujibu wa Kanuni ya 4 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mitandaoni), 2018, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ina jukumu la kutunza kumbukumbu za watoa huduma wote wa maudhui mtandaoni pamoja na kuchukua hatua stahiki za kisheria dhidi ya mtoa huduma yoyote wa maudhui mitandaoni atakayekiuka Kanuni za Maudhui Mitandaoni au sheria nyingine.

**1.3** Mtoa huduma ya maudhui mtandaoni, **GILLY BONNY ONLINE TV** anatuhumiwa kukiuka Kanuni za Maudhui Mitandaoni ambapo mnamo tarehe 13/05/2019 katika mtandao wa Youtube kupitia cheneli yake, ilichapisha maudhui yenye kichwa cha habari " ***Zitto Kabwe achafua hali ya hewa atuma waraka mzito kwa watawala***".

**1.4** Maudhui hayo yalichapishwa bila ya kuzingatia weledi weledi na mizania ya uandishi wa habari wakati wa uandaaji na usomaji wa Makala iliyodaiwa kutoka kwa Mhe. Zitto Zuberi Kabwe (MB) juu ya uamuzi wa Serikali wa kusitisha mradi maalumu wa Ukanda wa Uchumi wa Bagamoyo. Mtangazaji alisoma Makala hiyo kwa urefu juu ya hoja za Mbunge huyo kuwa Serikali imefaya uamuzi wa hovyo na usio na faida kwa nchi yetu bila kuweka maoni ya Serikali juu ya uamuzi wa kusitisha mradi huo.

**1.5** Aidha, mtangazaji hakufanya utafiti wa kutosha na hivyo hakuwa na uhakika wa alichokuwa akikisimulia juu ya taarifa ya msemaji wa serikali kuhusiana na mradi wa ujenzi wa barabara kutoka Dar es Salaam hadi Kibaha na mradi wa Bagamoyo. vile vile, hakuwa na taarifa ya ufafanuzi kutoka kwa msemaji wa Serikali juu ya maendeleo ya mradi huo wa barabara.

**2.0** Katika picha jongefu hiyo msimulizi aliendelea kusoma maneno yafuatayo, ***"...mradi wa Bagamoyo ungeleta mizigo yote ya Africa hapa Tanzania na reli mpya kupata biashara na hivyo kuleta faida ya uwekezaji, iweje sasa maamuzi yote yawe ya kufyeka na kuchelewesha miradi muhimu kama hii, hakika sina majibu ya maamuzi ya namna hii ila najua ni maamuzi ya hovyo ya siyo na faida kwa Taifa letu... na kuna mkanganyiko zaidi wa taarifa hizi mbili".***

**2.1** Kwa kuweka picha jongefu hiyo, **Gilly Bonny Online TV** imekiuka Kanuni Namba 7 (1)(a) na 7 (1)(b) ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mitandaoni), 2018 ambazo zinasomeka kama ifuatavyo;-

*7.-(1) A licencee of online radio and television intended for broadcasting over the public internet with the objective of informing, entertaining*

(a) *content streamed to abide to regulations governing the broadcasting services;.*

(b) *adhere to journalism ethics and professionalism*

**3.0 Wito wa kufika mbele ya Kamati ya Maudhui.**

Mnamo tarehe 22 Mei, 2019, Kamati ya Maudhui iliuandikia uongozi wa **GILLY BONNY ONLINE TV** wito wa kufika mbele ya Kamati kutoa utetezi wao kwa nini wasichukuliwe hatua za kisheria.

Tarehe 3 Juni, 2019, Saa 02:00 Asubuhi, uongozi wa **Gilly Bonny Online TV** uliwakilishwa na **Bw. Gilbert Boniface** na kufika mbele ya Kamati ya Maudhui kwa ajili ya kutoa utetezi wao kwa nini wasichukuliwe hatua za kisheria.

**4.0 Kusikiliza na Kuangalia Maudhui Mtandaoni ya GILLY BONNY ONLINE TV ya tarehe 13 Mei, 2019**

Kamati ya Maudhui na Uongozi wa **GILLY BONNY ONLINE TV** walisikiliza na kuangalia maudhui ya tarehe 13 Mei, 2019 yaliyowekwa na **GILLY BONNY ONLINE TV** katika chaneli yake ya Youtube ili kujiridhisha iwapo maudhui hayo yalikiuka Kanuni za Maudhui Mitandaoni.

**5.0 Maelezo ya Utetezi ya GILLY BONNY ONLINE TV.**

Uongozi wa **GILLY BONNY ONLINE TV** uliwasilisha utetezi wake na kukiri kosa na pia kuomba radhi.

**5.1** GILLY BONNY ONLINE TV wamedai kwamba kilichowapelekea wao kuchapisha taarifa hiyo ni kauli iliyotolewa na Serikali kupitia kwa Waziri wa Ofisi ya Mkakamu wa Raisi Muungano na Mazingira Mhe Jauari Makamba (MB) Kwamba serikali imesitisha mazungumzo na wawekezaji katika bandari ya bagamoyo, mradi ambao ungegarimu takribani Sh. Trilion 23, ambapo baadae kauli hiyo iliibua hisia miongoni mwa watanzania hasa wabunge wa upinzani hadi pale Waziri wa Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano Mhandisi Isack Kamwele (MB) alipoulizwa swali hilo

Majadiliano yaliendelea kwenye mitandao hadi Spika wa Bunge Mhe. Job Ndugai (MB) Aliposimama bungeni na kuitaka serikali ieleze kwa nini imesitisha mradi huo, ambapo Waziri husika alieleza na baadae Msemaj mkuu wa serikali akahitimisha kwa kutoa ufafanuzi sahihi.

5.2 **Gilily Bonny Online TV** ilidai kamba baada ya kuipata Makala hiyo waliihariri kwa kuondoa sehemu kubwa ya maneno kwa kuwa ilikuwa na maneno makali pengine yasingefaa kuifikia jamii kwa namna moja ama Nyingine, na kudai kwamba sio kweli kuwa waliipeleka hewani moja kwa moja bila kuhariri kabisa, Kuthibitisha hilo, Gilly Bonny Online TV iliambatanisha ushaidi wa Makala halisi ya Mhe! Zitto Kabwe kabla haijahaririwa na kuisoma Chanel yao.

5.3 Kuhusu kutozingatia mzania **Gilly Bonny Online TV** walidai kwamba Wakati upande wa Serikali unatolea ufafanuzi huo Bungeni wao tayari walishachapisha makala ile mtandaoni, pamoja na kwamba awali wakati wakiandaa walitafuta upande wa serikali bila mafanikio, ndio maana wanaomba Kamati iwasamehe kwa kurusha habari hiyo bila kuwa na uwiano.

5.4 **Bw. Gilbert Boiface** ambaye ni mmiliki na muanzilishi wa **GILLY BONNY ONLINE TV** aliendelea kuomba radhi na kuitaka kamati imhurumie na itambue kuwa **Gilly Bonny Online Tv** bado ni wachanga kwenye hii Tasnia ya Habari, hivyo wana mengi ya kujifunza kutoka kwa Kamti na wanatasinia wengine wanaoizunguka.

## 6.0 Majumuisho ya Utetezi wa GILLY BONNY ONLINE TV.

Katika kujumuisha utetezi wao, **Gilert Boniface** alizidi kuomba radhi na kusema kuwa **GILLY BONNY ONLINE TV** ni mara ya kwanza kutenda kosa hilo na kuahidi kuwa haitarudia tena kosa kama hilo.

## 7.0 Tathmini ya Kamati

7.1 Kamati ya Maudhui imebaini kwamba **GILLY BONNY ONLINE TV** imefanya kosa

kuchapisha habari isiyokuwa na mzania ni uzembe wa hali ya juu. pia taarfa yao ilijaa uchochezi na upotoshaji mkubwa.

**7.2** Kamati ya Maudhui imebaini kuwa utetezi wa **GILLY BONNY ONLINE TV** hauna msingi na kwamba msudhui waliyochapisha hayakuzingatia weledi.

**8.0 Ushauri wa Kamati kwa GILLY BONNY ONLINE TV.**

**8.1** Kamati inalengo la kuimarisha tasnia ya habari na utangazaji na kuwa haina nia ya kubana ubunifu wa watangazaji, bali inawataka wanahabari kuzingatia weledi Sheria, Kanuni na maadili ya uandishi wa habari.

Hata hivyo kutokana na kosa lililobainika, Kamati inaushauri Uongozi wa **Gilly Bonny Online TV kuweka usimamizi wa matangazo** ili kuhakiki maudhui yao ni salama kisheria kabla ya kuwekwa mtandaoni. Hatua hiyo itaiwezesha **Gilly Bonny Online** kuepuka kuvunja sheria na Kanuni za nchi.

**9.0 Uamuzi wa Kamati**

**9.1** Baada ya kusikiliza na kutafakari kwa kina maelezo ya utetezi yaliyotolewa na Uongozi wa **GILLY BONNY ONLINE TV**, Kamati ya Maudhui imeridhika kuwa **GILLY BONNY ONLINE TV** kupitia chaneli yake katika mtandao wa kijamii wa Youtube imekiuka kwa makusudi na uzembe mkubwa, Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui Mitandaoni), 2018.

**Hivyo basi**, Kamati ya Maudhui meamua yafuatayo:

**GILLY BONNY ONLINE TV** kulipa faini ya **Shilingi Milioni Tano na Laki Tano (TZS. 5,500,000.00)** tu kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa mujibu wa Kanuni Na. 18 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui Mitandaoni), 2018;

Pamoja na faini hiyo **GILLY BONNY ONLINE TV** inapewa Onyo Kali na, pia ina aamriwa kuomba radhi kwa Watanzania kwa kosa lililofanyika kupitia chaneli yao ya

Uamuzi huu umetolewa na kusomwa Dar es Salaam leo tarehe **04** mwezi **Juni** mwaka **2019**.

Haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu kwenye Baraza la Ushindani wa Haki Kibiashara (Fair Competition Tribunal – FCT) iko wazi ndani ya siku 21 (ishirini na moja) kuanzia leo.

.

**Uamuzi huu umesainiwa na:**

**Bi Valerie Ndeneingo-Sia Msoka**

.............................................................

**Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui**

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
20 BARABARA YA SAM NUJOMA
S. L. P. 474
14414 DAR ES SALAAM
TANZANIA

**PAMOJA NA WAJUMBE WA KAMATI YA MAUDHUI:**

1. **Bwana Joseph Method Mapunda** ..........................................
2. **Bwana Abdul Ramadhani Ngarawa**..................................
3. **Bwana Derek Kaitira Murusuri**........................................
4. **Bwana Jacob Gregory Tesha**............................................